

# Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina

# ukijua **mapema atakua** vizuri

## Hatua za Ukuaji

Watoto hukua, hujifunza na kuendelea kwa kasi tofauti. Mmoja anaweza kutembea mapema kuliko mwingine, huku mwingine anaweza kuwa wa kwanza kuongea. Tumia chati hii kama njia moja ya kuhakikisha iwapo mtoto wako anatimiza hatua za ukuaji katika miaka mitatu ya kwanza. Kumbuka kuwa kila mtoto ni tofauti. Ikiwa una maswali au wasiwasi kuhusu jinsi mtoto wako anavyoona, anavyosikia, anavyotembea, anavyowasiliana, anavyojifunza, anavyocheza au anavyoshirikiana na wengine, zungumza na daktari wako wa matibabu ya msingi au wasiliana na Shirika la Huduma za Maendeleo ya Watoto (CDSA, Children's Developmental Services Agency) la eneo lako. Ufanisi katika ukuaji na maendeleo ya mtoto wako huimarishwa kutokana na kuchukua hatua MAPEMA ikiwa una wasiwasi.

**Mwezi 1:** Anainua kichwa akiwa amelalia tumbo
Anaangalia/anakazia macho nyuso
Anajibu sauti



**Miezi 2:** Anatoa sauti - milio ya polepole na migugumo
Anafuata vitu kwa macho
Anainua kichwa kwa muda mfupi
Anatambua mikono yake

**Miezi 3:** Anatambua nyuso
Anainua kichwa juu na imara
Anaanza kuwa na tabasamu la kuvutia
Anaweza kustahimili uzito miguuni wakati miguu inawekwa kwenye sehemu ngumu
Anafuata vitu vinavyosonga

**Miezi 4:** Anatabasamu, anacheka na anaitikia polepole anapozungumziwa
Anageuka kutoka kulala kwa mgongo na kulalia ubavu au tumbo
Ananyoosha mkono kutaka kuchukua na kugonga vitu
Anatambua sauti na mguso wa mzazi

**Miezi 5:** Ananyoosha mkono kutaka kuchukua kitu, anakamata, na anaweka vitu mdomoni
Anabeba mikono juu ili kutaka kubebwa
Anacheza mchezo wa peek-a-boo
Anacheza kwa mikono na miguu

**Miezi 6:** Anaketi na kusimama kwa kusaidiwa
Anageuka pande zote mbili
Anageuka na kuangalia mahali sauti zinatokea
Anaiga sauti





**Miezi 7:** Anajibu hisia zinazoonyeshwa na wengine
Anatumia mikono kukagua, kupapasa, kugusa
Anatoa sauti mbalimbali

**Miezi 8:** Anapitisha vitu kutoka mkono mmoja hadi mwingine
Anavuta na kusimama
Anaanza kutambaa au kujivuta

**Miezi 9:** Anasema "Ma-ma" au "Ba-ba" kwa baba au mama
Anabadilisha ishara nawe (tabasamu)
Anabwabwaja au anaunganisha silabi
Anaitikia jina lake

**Miezi 10:** Anapunga mkono kuashiria kwaheri
Anatambaa vizuri kwa mikono na magoti
Anakunywa kutoka kwenye kikombe wakati kikombe kimeshikiliwa



**Miezi 11:** Anasema "Ma-ma" na "Ba-ba" kwa mzazi sahihi. Anatembea kwa kujishikilia kwenye vitu
Anakunywa kutoka kwenye kikombe na anaokota vitu vidogo

**Miezi 12:** Anatoa sauti na ishara rahisi.
Anatamka angalau maneno matatu
Anakuwezesha kujua kile anachotaka na asichokitaka

NC DEPARTMENT OF HEALTH AND HUMAN SERVICES
Division of Child and Family Well-Being

*Imeendelezwa kwenye ukurasa unaofuata*

www.ncdhhs.gov/itp-beearly

# ukijua mapema atakua vizuri

## Hatua za Ukuaji



**Miezi 13:**
Anasimama vizuri
Anainama ili kuchukua vitu na anaweza kupiga hatua chache

**Miezi 14:**
Anaiga shughuli za wengine
Anacheza na vitu mbalimbali vya kuchezea kama vile vigae, magari, vitabu, wanyama wa kushona na midoli
Anamwaga vitu vilivyo kwenye vyombo

**Miezi 15:**
Anacheza na mpira
Anatembea vizuri na anaweza kuinama
Anasikiliza haditihi
Anaweza kuonyesha sehemu zake za mwili

**Miezi 16:**
Anafungua kurasa za kitabu
Anaonyesha kupenda vidoli au vitu vingine
Anaweza kuwa na hasira anaposumbuliwa

**Miezi 17:**
Anajifunza njia sahihi ya kutumia vitu kama vile simu
Anapenda michezo ya kuigiza
Anapenda kuendesha midoli

**Miezi 18:**
Anaweza kusema maneno 10 hadi 20
Anaomba usaidizi
Anatumia neno moja kusema anachotaka/anachohitajika
Anachorachora na penseli ya rangi
Anaonyesha mapenzi, anabusu
Anafuata maelekezo rahisi.
Anaweza kutembea akirudi nyuma



**Miezi 19:**
Anatumia kijiko au uma
Anaweza kukimbia
Anatupa mpira kwa mkono
Anafurahia kusaidia kufanya kazi nyumbani

**Miezi 20:**
Anaweza kuvua nguo mwenyewe
Anaweza kuelewa maneno 200

**Miezi 21:**
Anaunganisha maneno kama vile “ninataka chupa” na “nenda kwaheri”
Anaweza kupanda ngazi hatua kwa hatua
Anaweka malengo rahisi kama vile mahali pa kuweka midoli

**Miezi 22:**
Anapiga mpira mbele
Anafuata ombi la hatua mbili kama vile “chukua kidoli na unifetee”

**Miezi 23:**
Anaweza kutambua picha rahisi kwenye kitabu
Anajitambulisha kwa jina - anatumia “mimi/yangu”
Anaweza kufungua kabati na vikasha
Anatumia maneno "habari," "kwaheri," na “tafadhali” akikumbushwa

**Miezi 24:**
Atajibu maswali rahisi kama vile “Hii ni nini?”
Anataja angalau sehemu sita za mwili
Anatumia vifungu vya maneno mawili na matatu
Anapiga mpira kwa mguu
Anapanda na kushuka ngazi hatua kwa hatua
Anafuata zamu anapocheza na wengine



**Wakifikisha umri wa miaka miwili,** watoto huzungumza zaidi, wakitumia vifungu vya maneno mawili na matatu na kuomba vitu kama vile “niongezee juisi.” Wana msamiati wa maneno 50 hadi 100 na wanaelewa maneno 250 hadi 300. Wanaweza kujilisha na kufungua kabati na vikasha. Wanapenda pia kutenganisha vitu, kugundua mazingira yao na kuiga wazazi wao na watoto wengine. Tabia za kawaida za kijamii na kihisia ni kuonyesha mapenzi, kucheza peke yao na kuona aibu mbele ya wageni. Watoto wenye umri wa miaka miwili huwa na misimamo mikali, kwa hivyo wanaweza kuwa na hasiri.

**Wakifikisha umri wa miaka mitatu,** watoto hujitegemea zaidi. Kivitendo, wanaweza kupanda na kushuka ngazi na kuvaa viatu. Kwa kuweza kusema sentensi za maneno matatu hadi matano, wanaweza kurudia vina, kuelewa sentensi nyingi na kusema majina na umri wao. Watoto wenye umri wa miaka mitatu wanaweza kucheza mchezo wa kuigiza na midoli, wanyama na watu. Wanaweza kucheza michezo rahisi na watoto wengine, kutaja angalau rangi moja kwa usahihi na kuendesha baiskeli ya magurudumu matatu. Watoto wenye umri wa miaka mitatu huonyesha hisia mbalimbali.

Ingawa nyakati kamili za kufikia hatua hizi zinaweza kuwa tofauti kwa watoto, hatua hizi zinaweza kutumika kama mwongozo unapomtazama mtoto wako akikua na kukomaa.

Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya NC • www.ncdhhs.gov • Idara ya Ustawi wa Watoto na Familia • Kitengo cha Suluhu za Mapema • NCDHHS ni mwajiri na mtoa huduma asiyebagua mtu yeyote. • 12/13, Ilisasishwa 4/22, 1/23, 5/23, 10/23, 7/24.

NC DEPARTMENT OF HEALTH AND HUMAN SERVICES
Division of Child and Family Well-Being

www.ncdhhs.gov/itp-beearly